

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MANISPAA
(SURA YA 288)**

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)

**SHERIA NDOGO YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA
MUSOMA (ADA YA UZOAJI, UTUPAJI TAKA NA USAFI WA
MAZINGIRA) ZA MWAKA 2017**

- | | | |
|----|--|-------------------------|
| 1. | Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Usafi wa mazingira za Manispaa ya Musoma za mwaka 2017. | Jina |
| 2. | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma. | Eneo la Matumizi |
| 3. | Katika Sheria Ndogo hizo isipokuwa itakapoeleza vinginevyo
“ada” maana yake ni malipo yanayotakiwa kufanywa na kampuni, viwanda, mtu binafsi, Taasisi kwa ajili ya kupima Afya au kufanyiwa uchunguzi wa kiafya kwa mfanyakishara wa chakula, mhudumu wa biashara ya chakula au mfanyakazi wa kiwandani ndani ya Halmashauri ya Manispaa:
“adha” maana yake ni hali yoyote mbaya yenye kuleta madhara juu ya afya ya watu kwa ujumla;
“Afya” maana yake hali timilifu ya kimwili, kiakili na kijamii na wala sio tu kuwa na ugonjwa au kilema;
“Afisa mwidhiniwa” maana yake Afisa ye yote aliyeulewa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;
“Bafu” maana yake chumba maalum kilichojengwa kwa madhumuni ya kuogea;
“Chakula” maana yake kitu chochote kinacholiwa na binadamu na inajumuisha maji na dawa;

“Choo bora” maana yake choo cha lindi chenye, shimo lililojengwa madhubuti au choo cho chote cha maji chenye sakafu imara, banda imara la kudumu, imeezekwa, kina mlango imara kama cha lindi kimeongezwa bomba la kutoa hewa chafu na chenye mfuniko kwenye tundu la choo.

“Chukizo la afya: maana yake kitu cho chote kinachowenza kuleta kinyaa machoni kwa kuona, kunusa, hewa chafu, madhara au kuhatarisha Afya za binadamu na wanyama; | Tafsiri |
- “Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Musoma;
“Jengo la biashara” maana yake jengo lo lote lililojengwa na kuidhinishwa na mamlaka kufanya biashara iliyokusudiwa;

“Kaya” maana yake familia moja baba, mke na mtoto au watoto inayoishi aidha kwenye nyumba nzima au ndani ya chumba kimoja kwenye maeneo ya kata za Halmashauri;

“Kikundi cha usafishaji” maana yake kikundi cho chote cha watu kinachosajiliwa kufanya shughuli za usafi wa mazingira na hasa za udhibiti wa uharibifu wa mazingira katika maeneo ya Manispaa ya musoma

“Kituo cha maji machafu” maana yake sehemu maalum iliyotengenezwa Kwa ajili ya ukaguzi wa mfereji ambacho kina mfuniko usioruhusu hewa kutoka (Airtight cover);

“Kituo cha taka” maana yake kizimba cha taka au chombo maalum cha kuhifadhi taka, kasha “refuse bin container” ambayo imewekwa na Halmashauri kwa madhumuni ya jamii inayoishi jirani kuweka taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi kwenye jalala la taka ngumu la Manispaa.

“Kutupa taka ngumu” maana yake kukusanya taka zote zinazozalishwa na familia, kampuni, sehemu ya biashara, ofisi, taasisi n.k. na kuzipeleka hadi kwenye jalala la Halmashauri, jalala kuu (final disposal site) kwa madhumuni ya kuzitupa ndani ya jalala mujibu wa kanuni zilizowekwa na mji.

“Mabwawa ya maji taka” maana yake mabwawa yaliyojengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi na kutakasa maji taka yanayotokana na kuosh vyombo, kufua nguo, kuosha nywele au shughuli zo zote za nyumbani na viwanda;

“magonjwa ya milipuko” maana yake ni magonjwa yanayotokea kwa muda mfupi na kuathiri watu wengi yanayoweza kutolewa amri ambayo ni Acute flaccid, kupooza, kipindupindu, kuhara, Louse bare typhus, (relapsing) fever, suruwa, homa ya uti wa mgongo, pepopunda, tauni, kichaa cha mbwa na homa ya matumbo:

“Mazalia ya wadudu” maana yake sehemu anbayo wadudu hufanya mazalio au kuishi kwa minajiri ya kufanya mzunguko wa maisha na baadae huleta maafa;

“Mifugo” maana yake ng’ombe, punda, nguruwe, mbuzi, kondooau kuku na wanyama wengine wote wafugwao majumbani;

“Mkurugenzi” maana yake Mkurugenzi wa Manispaa au Afisa ye yote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya M kurugenzi;

“Mzalishaji wa taka ngumu” maana yake mtu ye yote, kaya, taasisi, biashara au kiwanda ambaye katika kutekeleza shughuli zake za kila siku huzalisha taka ngumu;

“Mtando wa maji taka” maana yake mfumo wa bomba kuu lililojengwa kwa madhumuni ya kupokea na kusafirisha taka miminika toka kwenye mifereji ya

maji na kuyapeleka kwenye mabwawa ya maji taka;
“Mzalishaji wa maji taka” maana yake mtu, shirika, kiwanda au taasisi ambapo shughuli zake kwa namna yo yote ile huzalisha maji taka;
“Pipa la taka” maana yake chombo cho chote kilichokubakiwa na halmashauri kitumike kama chombo cha kuhifadhia taka ngumu zinazozalishwa majumbani, sehemu za biashara, sehemu za biashara, maofisini na ni pamoja na chombo maalum kunachobebwa na gari la takataka;
Taka ngumu” maana yake kitu cho chote kwa jamii inayohusika, uwepo wake katita eneo husika unaweza kusababisha machukizo ya kiafya na kuhatarisha afya ya jamii;

“Taka za majumbani” maana yake mabaki ya vyakula, maganda ya matunda, majivu, marapurapu ya nguo, karatasi za aina mbalimbali, vinyesi vya mifugo, taka za bustani na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa;

“Taka ndogo ndogo” maana yake mabaki ya vocha za simu, chupa za maji, chupa za juisi, maganda ya pipi, chocolate, ice cream, pakiti za sigara, vichungi vya sigara, vizibo vya chupa, maganda ya matunda, miwa, mahindi, machungwa, mananasi, masalia ya magunzi, mbogamboga, na magazeti na karatasi za aina mbali mbali na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa;

“Ufuganji wa ndani” maana yake ni kuwa na banda la mifugo na ulishaji wa mifugo kufanywa ndani ya mipaka ya nyumba.

“taka za biashara” maana yake ni aina yo yote ya taka ambazo kupatikana au hutokana na uzalishaji wa shughuli mbalimbali za kibashara;
“taka za viwanda” maana yake aina yo yote ambazo hutokana au uzalishaji wa shughuli mbalimbali viwandani;

“taka za hatari” maana yake aina yo yote ya taka ambayo kwa njia Fulani hubaki kwenye mazingira na hatima yake ni kusababisha madhara kwa afya ya jamii ikiwa ni pamoja na taka zitokanazo na shughuli za hospitali “x-ray, films, radio active materials”, vitu vyenye ncha kali kama sindano, chupa au taka zitokanazo na shughuli za uzalishaji viwandani kama vile (dry batteries), mecury, madawa mbalimbali, mabasi, vyuma, kemikali, gesi mbalimbali;

“taka miminika” maana yake maji yaliyokwisha tumika au kuchafuliwa kwa namna yo yote ile ambayo yanajumuisha maji machafu toka chooni, bafuni, jikoni, viwandani, maji yaoshewayo vyombo, maji yaliyofuliwa nguo, kuosha nywele, kuoshea vyakula na yaliyopigiwa deki;

‘taka za maofisini’ maana yake karatasi na aina yoyote ya uchafu utakaozalishwa na mwenye ofisi

“Upimaji wa afya” maana yake ni hali ya mtu kupima afya yake kwa kuchukuliwa vipimo vya ndani na nje ya mwili ili kubaini kuwepo kwa

vijidudu vya wagonjwa vinavyoweza kuleta maambukizi;
“Ugonjwa wa kuambukiza” maana yake ugonjwa wo wote uambukizwao toka
kwa mtu na mtu au mtu kwa mnyama mfano kifua kikuu, Brucellosis, kimeta,
safura, surua, kipindupindu au uti wa mgongo.

4. Afisa ye yote aliyeidhinishwa na Halmashauri atakuwa na uwezo wa kuingia na
kukagua eneo lolote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa
ya musoma kwa nia ya kuangalia kero /chukizo na kutoa maelekezo ya
kuondoa machukizo/ kero hizo

5 (1) Ni marufuku kutupa takataka au uchafu wowote au kuacha kuwepo
takataka au uchafu kwenye nyumba, biashara, kiwanja, mfereji wa maji ya
mvua, barabara au mahali po pote pasipotengwa kwa shughuli hiyo.

(2) Ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba ya kuishi, duka la biashara, ofisi
iliyoko ndani ya Jiji kuhakikisha kwamba-

- (a) Ana pipa lenye mfuniko litakalotumika kutupia taka ngumu; na
- (b) Anasafisha mfereji wa maji ya mvua uliopita karibu na nyumba, duka,
ofisi yake na mfereji na maeneo yanayozunguka nyumba, duka, ofisi
yake yanakuwa safi muda wote;

(3) Gari lolote lilibeba taka ngumu linatakiwa liwe limefunkwa kiasi cha
kuzuia taka ngumu zisionekane wala kumwagika chini na kuleta adha
kwa watu na uchafuzi wa mazingira kwa ujumla.

(4) Kila mwenye basi litakaloingia eneo la Halmashauri ya Manispaa ya
Musoma atawajibika kuwa na chombo cha kuhifadhia taka na kuhakikisha
kwamba kila abiria anatupa taka humo.

(5) Itakuwa ni kosa kwa mwenye basi dereva au kondakta iwapo abiria aliye
ndani ya basi lake atatupa kitu chochote barabarani au stendi.

(6) Mwenye basi au dereva au kondakta atawajibika kulipa faini ya shilingi
elfu ishrini na tano baada ya kujaziwa fomu ya ilani na Afisa wa Manispaa

6. (1) Ni wajibu wa kila kaya, mwenye biashara, ofisi au kiwanda kuhakikisha
kwamba inalipa ada ya uzoaji taka kwa viwango vilivyoainishwa kwenye
jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi ikiwa ni gharama ya kusafirisha
taka ngumu kutoka kwenye nyumba yake hadi sehemu iliyotengwa
maalum kwa ajili ya kutupa taka ngumu (Dampo)

Ada ya uzoaji taka

(2) Manispaa inaweza kumteua mtu ye yote, kikundi cha watu, kampuni au
taasisi kukusanya ada ya uzoaji taka kwa niaba yake

Kusimamia usafi na
uzoaji taka kisha
kukunya ada ya uzoaji
taka

7. Kila mmiliki wa nyumba katika eneo la Halmashauri ya Manispaa ya Musoma anatakiwa kuwa na choo bora na safi kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo
8. (1) Utakuwa ni wajibu wa mwenye nyumba kuunganisha choo cha maji na maji machafu toka kwenye makaro kwenye mtandao wa maji taka, iwapo atashindwa kufanya hivyo atatakiwa aelekeze uchafu huo katika mashimo ya maji taka.
(2) Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni, baa, klabu, gereji au shughuli yo yote inayokusanya watu wengi kwa pamoja anatakiwa kuweka na kutunza vyoo vya kutosha kwa jinsia za kiume na kike.
(3) Kila Kata kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi vya Usafi na kusimamia vikundi hivyo.
(4) Iwapo Halmashauri itagundua kuwa nyumba yo yote haina choo au choo kilichopo hakifai kwa matumizi ya binadamu, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuchukua hatua yo yote inayoona inafaa ikiwa ni pamoja na kuzuia nyumba hiyo isitumike hadi choo kitakapojengwa au kurekebishwa
9. Ni marufuku kwa mtu ye yote kumwaga, kutiririsha maji taka katika mtaa, uchochoro, eneo la wazi, mtaro ulio wazi au mashimo yasiyoruhusiwa
10. (1) Endapo kutatokea chukizo la kiafya kutokana na maji taka au choo katika nyumba yenye mpangaji zaidi ya mmoja na iwapo mwenye nyumba hawezikupatikana kwa haraka, Halmashauri itaweza kuamuru wapangaji kuondoa chukizo hilo na kulipa faini kwa mujibu wa sheria ndogo hizi.
(2) Ni marufuku mtu ye yote kuendesha biashara ya nyumba ya wageni au hosteli ya wanafunzi bila ya kibali cha Halmashauri.
(3) Kibali cha hosteli ya wanafunzi au nyumba ya kulala wageni kitatolewa baada kuthibitisha yafuatayo:-
a) Utoshelezaji wa vyoo /bafu kwa jinsi zote;
b) uondoshaji wa taka ngumu na taka miminika;
c) uimara wa jengo;
d) mwanga na hewa ya kutosha;
e) usafi wa jumla wa jengo;
f) nafasi ya kutosha;
g) vifaa na samani za kutosha.
11. Kila mwenye nyumba anawajibika kuhakikisha kuwa hakuna mazalia ya wadudu kama vile mbu kwenye nyumba yake au karibu na nyumba yake kwa kuondoa maji yaliuokusanyika, kufyeka majani au kuharibu kitu cho chote kinachowezwa kuwa mazalia ya wadudu.

Biashara

12. Ni marufuku kwa mtu ye yote kufanya biashara ya aina yo yote kwenye maeneo ambayo hayajatengwa rasmi kwa shughuli za biashara ya aina hiyo.
13. (1) Ni marufuku kwa mtu ye yote kuuza vyakula kwenye eneo lolote la Halmashauri ambalo halijatengwa kwa matumizi ya kuuzia vyakula. Uthibiti uuzaji wa vyakula
- (2) Mtu ye yote anayetaka kufanya biashara ya kuuza chakula atatumma maombi kwa Halmashauri na iwapo Halmashauri itaridhika na maombi yake atapatiwa kibali cha eneo la kuuzia chakula.
- (3) Halmashauri inaweza kufuta kibali kilichotolewa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) iwapo mtu aliyepewa kibali atakiuka masharti ya kibali hicho.
14. (1) Ni marufuku kwa mtu ye yote kukata au kuharibu mti wa aina yo yote ndani ya Halmashauri bila kibali. Ukataji wa miti
- (2) Mtu ye yote atakayekata na kuharibu mti wo wote atawajibika kulipa gharama za kupanda na kukuza mti mwengine.
15. Ni marufuku kwa mtu ye yote kujisaidia haja ndogo na haja kubwa ovyo katika eneo ambalo siyo choo. Kujisaidia hovyo
16. Kila mmiliki wa hoteli, migahawa, baa za aina zote za kigeni au kienyeji, bucha, sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, grosari au eneo lo lote linaloshughulika na vyakula vilivyotengenezwa kwa ajili ya kuuza atawajibika kuhakikisha kuwa wahudumu wake wamepimwa afya zao kabla ya kuanza kazi na atahakikisha kuwa wanapimwa afya zao kila baada ya miezi sita.
17. (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote:- Wajibu wa kutunza vyanzo vyamaji
- (a) Kunawa, kuoga au kufulia nguo au kunywesha mifugo karibu au kwenye vyanzo vyamaji kama vile chemchem, kisima, ziwa au chanzo kingine cho chote cha maji, au kunywesha mifugo kwenye chanzo cha maji kinachotumika kwa matumizi ya nyumbani.
- (b) Kuacha shimo la maji machafu wazi au kumwaga maji kutapisha au kuruhusu kufurika choo, karo, kuruhusu kupasuka au kuziba bomba la maji taka toka ndani ya nyumba na kuyatiririsha kwenye maeneo ya barabara au sehemu nyingine na kusababisha adha.
- (c) Kujenga boma la mifugo karibu au kuruhusu mkojo au maji

- (d) Kufuga mfugo wa aina yo yote bila kibali cha Halmashauri au
- (e) Kuacha mifugo au kusababisha mifugo kuzurura ovyo mitaani, barabarani au kuchungwa kwenye eneo lolote lisilorusiwa.
- (2). Mfugo wowote utakaokutwa ukizurura au kuchungwa kwenye eneo lisilorusiwa utakamatwa na Halmashauri na mwenye mfugo atalazimika kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini, gharama za kukamata mifugo shilingi elfu tano kwa kila mfugo na shiilingi elfu kumi kwa siku kwa kila mfugo utakaokamatwa na kutunzwa katika Yard ya Halmashauri.
- (3) Mfugo wo wote utakaoshindwa kukombolewa ndani ya muda wa siku saba utauzwa kwa njia ya Mnada ili kulipia faini gharama za ukamataji na utunzaji wa mfugo .
- (4) Hairuhusiwi kabisa kufuga aina yoyote ya wanyama kama vile ng'ombe, mbuzi, nguruwe na wanyama wengine kwenye eneo la msongamano wa nyumba za makazi.
- (i) Kwa namna yo yote ile ufugaji ni lazima ufanyike kwa kuzingatia matumizi ya ardhi ya eneo husika na kwa kibali maalumu kitakachotolewa na Halmashauri na si vinginevyo.
- (5) Kila mfugaji wa ng'ombe, mbuzi, kuku, nguruwe na wanyama wengine wafugwao atawajibika kukusanya na kuhifadhi uchafu wowote utokanao na wanyama hao kama vile kinyesi, manyoya, utumbo (baada ya kuchinjwa) na uchafu utokanao na ufugaji huo mfano nyasi au mabaki ya vyakula kwa namna ambayo inakubalika kwa Halmashauri na ambayo haitaleta kero na maudhi kwa jamii.
18. Ni marufuku kwa mtu ye yote:-
- (a) Kuegesha gari bovu au kufanya matengenezo ya magari katika maeneo ya wazi , pembedi mwa barabara au katika eneo lolote liloziiliwa na Halmashauri
- (b) Kuosha gari kwenye eneo ambalo halijatengwa rasmi kwa kazi hiyo; au
- (c) Kupanga bidhaa kwenye njia ya wapitao kwa miguu; uchocholo, kwenye pavement na maeneo ya wazi.
- (d) Ni marufuku kwa mtu ye yote kuchimba kokoto, mawe au mchanga katika eneo la Halmashauri bila kibali.
- (e) Ni marufuku kwa mtu ye yote kutengeneza au kuparua samaki katika maeneo yasiyoruhusiwa .

- (f) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha biashara ya upulizaji dawa za kuuwa wadudu /wanyama waharibifu katika nyumba yeyote au mahali popote bila cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na bila kuwa na leseni ya Halmashauri
- (g) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha biashara ya upulizaji dawa za kuuwa wadudu /wanyama waharibifu katika nyumba yeyote au mahali popote bila cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na bila kuwa na leseni ya Halmashauri
- (h)) Itakuwa ni kosa kwa mtu yoyote kuweka mtambo, mashine, gari au pipipiki inayochafua hewa kwa kutoa moshi mzito kutokana na uchakavu wa chombo hicho
19. Halmashauri inaweza kuteua mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi kusimama utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi
20. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi za kitanzania laki mbili nausiozidi shilingi za kitanzania milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja faini na kifungo. Adhabu
21. (i) Kila mwenye nyumba na mtumiaji wa sehemu ambapo taka za viwandani zinazalishwa au taka za Hospitali au taka zozote zinazozalishwa atapaswa kuzitunza na kuhakikisha kuwa anaziondoa kwa umakini kama atakavyoelekezwa na Halmashauri
- (ii) Itakuwa ni kosa kwa mtu yoyote kuweka mtambo, mashine, gari au pipipiki inayochafua hewa kwa kutoa moshi mzito kutokana na uchakavu wa chombo hicho
22. Kutakuwepo na ada ya kutupa taka katika dampo kwa kila mtu, wakala, taasisi za kijamii, kiwanda, taasisi zisio za kiserikali na taasisi nyingine zozote ambazo zimeruhusiwa kuzoa na kutupa taka kwa niaba ya Halmashauri. Viwango vitakavyotumika ni vile vilivypangwa na Halmashauri kwa mujibu wa sheria hii.
23. Madeni ya Ada ya kuzoa Taka yaliyoainishwa kwenye sheria ndogo hizi yatakusanywa kutoka kwa mmiliki kwa kumpelekea hati ya madai kwa maandishi na iwapo atashindwa kulipa kwa muda wa siku saba (7) Halmashauri au mtu yeyote aliyeidhinishwa anaweza kufungua kesi ya madai. Mahakama itakaporidhika juu ya deni mdaiwa ataamriwa kulipa deni hilo

- pamoja na adhabu ya 50% ya deni analodaiwa.
- 24 Kila mmiliki wa nyumba katika eneo la Halmashauri ya Manispaa anatakiwa kuwa na choo bora na safi kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo, choo ambacho kina shimo lisilopungua urefu wa mita 3 kwenda chini na upana wa shimo usiopungua mita 1 , shimo la choo lazima liwe na bomba la kutolea hewa chafu na wavu kwa kuzuia nzi, Sakafu itengenezwe kwa mchanganyiko wa zege na saruji na isiruhusu maji kunyonywa , kuta ziwe za tofali na sisilibwe kwa saruji na paa liwekwe la kudumu.
- 25 Vitajengwa vyoo vya umma katika maeneo ambayo Halmashauri itaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo
- 26 Vyoo vya umma vitamilikiwa na Halmashauri na vitalipiwa ada na ushuru kama itakavyoelekezwa na Halmashauri.
- 27 Kutakuwa na vyoo vya mda vitakavyojengwa kwa ajili ya kutumika kwa muda maalum kwa matumizi ya watu sehemu zenyen ujenzi , Sherehe au sehemu yeoyote itakayokutanisha watu kwa muda maalim na vyoo hivyo vitajengwa kwa kibali kitakachotolewa na Halmashauri.
- 28 Samaki watawekwa kwenye meza zilizojengwa maeneo ya sokoni na wauzaji watalazimika kuva mavazi rasmi yenyen rangi nyeupe na kofia (Apron).
- 29 (1) Maduka yote ya kuuza nyama (Bucha) lazima yawe kwenye majengo ya kudumu yawe na maji wakati wote , mashine za kukatia nyama, makabati ya vioo majokofu ya kuwekea nyama sehemu za mizani, pipa la taka, wavu wa kuzuia nzi, vazi rasmi lenye rangi nyeupe pamoja na kufia nyeue (Apron) livaliwe wakati wote na muuzaji wa nyama .
- (2) Mtu ye yote anayetaka kuchimba mchanga, kokoto au mawe katika eneo la Halmashauri atatumwa maombi yake kwa Mkurugenzi pamoja na kulipa ada ya maombi hayo kwa viwango vitakavyopangwa na Halmashauri.
- (3) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukataa maombi yoyote iwapo itaona kuwa uchimbaji wa kokoto, mawe au mchanga utakuwa na athari za kimazingira

Wajibu wa
kupima Afya

**JEDWALI LA KWANZA
ADA YA UKUSANAJI NA UZOAJI TAKA KWA MWEZI**

	MAENEKO YA UZALISHAJI WA TAKA NGUMU	MWIGOBERO, MUKENDO N KITAJI NA IRINGO	MWISENGE KAMNYONGE NYASHO NYAKATO BWERI NA NYAMATARE	KIGERA, MAKOKO ,BUHARE KWANGWA RWAMLIMI
		TSHS	TSHS	TSHS
1.	Makazi (kwa familia)	1,000	800/-	500/-
2.	Nyumba ya kupangisha	1,000	800/-	300/-
3.	Ofisi	2,000/-	1000/-	500/-
4	BENKI: Benki ya Biashara	10,000	5,000	1,000/-
5	Duka la kubadilisha fedha	5,000	2,000	500/-,
6	VYAKULA NA VINYWAJI Hoteli	10,000	5,000	2,000
7	Mgahawa	5,000	1,000	500/-,
8	Café (Food, snacks & soft drink)	8,000	3,000	1500/-
9	Duka la vyakula na vinywaji (Grocery)	8,000	3,000	1500/-
10	Baa (pombe), vinywaji baridi na vitafunwa)	8000	3,000	1500/-
11	Baa na Mgahawa	10,000	5,000	2,000
12	Baa na Nyumba la kulala wageni	10,000	5,000	2,000
13	Baa, nyumba ya wageni na ukumbi wa starehe	10,000	5,000	2,000
14	Baa na ukumbi wa starehe	8,000	3,000	1500/-
15	Baa, ukumbi wa starehe na mgahawa	10,000	5,000	2,000
16	Duka la kuuza “Ice cream”	5,000	2,000	500
17	Bucha ya nyama na samaki wabichi	8,000	3,000	1,000
18	DUKA (JUMLA NA REJAREJA)			
19	*Vyakula na bidhaa mchanganyiko jumla	10,000	5,000	2,000
20	*Nguo	8,000	5,000	2,000
21	Vifaa vya umeme (Electronic & electrical appliances)	5,000	2,000	1,000/-
22	*Vifaa vya ujenzi (Hard ware stores)	8,000	3,000	1,000
23	*Vitabu, shajara na vitu vya zawadi	5,000	2,000	1,000
24	*Sonara na vipodozi (Jewelry & Machinery)	10,000	5,000	2,000
25	*Duka la samani(Furniture & machinery)	10,000	5,000	2,000
26	*Vinywaji na Pombe kali	8,000	3,000	1,000

	(Beverages and Liquor stores)			
27	*Vipuri na vifaa (Spareparts and tools)	8,000	3,000	1,000
28	Duka la vifaa chakavu (junk shops)	10,000	5,000	2,000
29	Duka la reja reja	8,000	3,000	1,000
	KARAKANA NA VIWANDA			
30	Fundi selemala	10,000	5,000	2,000
31	Karakana ya chuma (metal W/shop)	8,,000	3,000	1,000
32	Karakana ya Magari (motor garages)	10,000	5,000	2,000
33	Sonara na uhunzi wa vito (jewely and black smiths)	10,000	5,000	2,000
34	Shughuli za vioo (glass works)	10,000	5,000	2,000
35	Mchapishaji (Printers)	8,000	3,000	1,000
36	Mashine ya mbao kwa ujao wa mita 1 (saw mills per M ³)	8,000	3,000	1,000
37	Viwanda vikubwa : kwa tani moja ya taka : kwa ujazo w mita za mraba mmoja Viwanda vidogo : kwa tani moja ya taka : kwa ujazo w mita za mraba mmoja	20,000/- 10,000	10,000/- 5,000	5,000/- 2,000/-
38	Umembe na Matengenezo ya elecktoniki (electrical and electronic repairs)	8,000	3,000	1,000
39	Magurudumu na matengenezo	5,000	2,000	1,000
40	BIASHARA NDOGO NA SEKTA ISIYO RASMI			
41	Fundi cherehani	2,000	1000	500
42	Selermala	2,000	1,000	500
43	Fundi viatu (cobler /Shoe repai)	2,000	1,000	500
44	Saluni ya Nywele	2,000	1,000	500
45	Dobi and Dry cleaner	2,000	1,000	500
46	Genge kwa meza moja	5,000	3,000	2,000
47	Huduma ya shajara	5,000	3,000	1,000
48	Huduma ya “internet”	5,000	3,000	1,000
49	HUDUMA ZA AFYA (Taka zisizokuwa za hatari)			
50	Duka la dawa baridi	10,000	5,000	2,000
51	Maabara ya vipimo binafsi	10,000	5,000	2,000
52	Zahanati binafsi	8,000	3,000	1,000
53	Madawa asilia	5,000	2,000	1,000
54	Hospitali binafsi	10,000	5,000	2,000
55	Hospitali ya rufaa	20,000	10,000	5,000

56	TAASISI ZA MAFUNZO (Kituo cha kulelea watoto, shule za kutwa na Vyuo binafsi)	20,000/-	10,000/-	5,000/-
57	SHULE ZA KUTWA ZA BINAFSI	20,000/-	10,000/-	5000/-
58	VITUO VYA MAFUTA			
59	Kituo cha kikubwa cha mafuta	50,000	20,000	10,000
60	Kituo kidogo cha mafuta	30,000	15,,000	10,000
61	Kituo cha mafuta ya taa	10,000	8,000	5,000
62	Kituo cha kuuzia gasi	10,000	5,000	2,000
63	Kibanda cha kuuzia mkaa	10,000	5,000	2,000
64	HUDUMA NYINGINEZO			
65	Jumba la starehe na klabu	10,000	5,000	2,000
66	Ofisi za ulinzi	5,000	3,000	1,000
67	Duka la simu, Kampuni ya simu kwa mnara wa mawasiliano (Mobile – phone companies	10,000	5,000	2,000
68	TAKA ZENYE UJAZO MKUBWA (BULKY AND BUNDLE WASTE)			
69	Taka za viwandani kwa tani moja	25,000	25,000	25,000
70	Taka za uvunjaji jengo kwa tani moja (Demolition Debris per ton)	20,000	10,000	5,000

- Ada ya kupima maziwa
- Ada ya matumizi ya dampo

Tshs 1000 kwa siku
Tshs 5000 kwa trip moja .

Nembo ya Halmashauri ya Manispaa ya Musoma imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio liliopitishwa katika Kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kilichofanyika tarehemwezimwaka 2017 mbele ya:

.....
**MH: PATRICK WILLIUM GUMBO
MSTAHIKI MEYA
HALMASHAURI YA MANISPAA
MUSOMA**

.....
**FIDELICA G. MYOVELLA
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MANISPAA
MUSOMA**

NAKUBALI,

TAREHE
DODOMA
**MH. GEORGE B. SIMBACHAWENE (Mb)
WAZIRI WA NCHI – OR - TAMISEMI**